

# JARIDA LA MAKAMBAKO YETU

www.makambakotc.go.tz | Kitengo cha Mawasiliano Serikalini | Halmashauri ya Mji Makambako

## MIAKA 3 YA

DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

**RAIS WA AWAMU YA SITA WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**





# MIAKA 3 YA
# DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
# HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



## DIVISHENI YA ELIMU SEKONDARI - MIAKA 3 YA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN



SHULE MPYA YA SEKONDARI YA MBUGANI-KITANDILILO

**Na. Lina Sanga**

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 divisheni ya elimu sekondari imepokea jumla Mil. 92. 5 kutoka Serikali Kuu,kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa na maabara katika shule za sekondari 5.

Shule hizo ni shule ya sekondari Kitandililo jumla ya mil.37.5 zimetumika kwa kazi ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa matatu.

Mil. 30 zimetolewa kwa shule ya sekondari Maguvani kwa ajili ya ukamilishaji wa boma la maabara.

Mil. 12.5 zimetolewa kwa shule ya sekondari Makambako kwa ajili ya ukamilishaji wa boma la darasa.

Mil. 12.5 zimetolewa kwa shule ya sekondari Mukilima kwa ajili ya ukamilishaji wa boma la darasa.





# MIAKA 3 YA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO

## DIVISHENI YA ELIMU YA AWALI NA MSINGI




MADARASA 2 NA OFISI 1 -SHULE YA MSINGI IKWETE (SHULE KONGWE)


**Na. Lina Sanga**

Katika Mwaka wa fedha 2023/2024 divisheni ya elimu msingi imepokea jumla ya Mil. 311 kutoka Serikali kuu na kupitia mradi wa EP4R kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya madarasa ,matundu ya vyoo na bweni la watoto wenye mahitaji maalum shule ya msingi Idofi.

Kupitia fedha hizo jumla ya madarasa 10 yamejengwa katika shule kongwe 4 ambazo ni shule ya Msingi Makambako,Manga,Mawande na Ikwete na kila shule ilipokea mil. 45 kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na shule ya msingi Mshikamano ilipokea kiasi cha mil. 85 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 2 na matundu ya vyoo 5 kupitia fedha za mradi wa EP4R na madarasa hayo yanatumika kwa shule zote.



## MIAKA 3 YA
## DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
## HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



Aidha jumla ya matundu ya vyoo 32 yamejengwa katika shule za msingi 5 ambazo ni pamoja na shule ya msingi Mshikamano matundu 5 ya vyoo,Bwawani matundu 7 ya vyoo ,Maendeleo matundu 11 ya vyoo ,Juhudi matundu 5 ya vyoo na Ushindi matundu 4 ya vyoo.

Pia,shule ya msingi Idofi ilipokea mil. 20 kutoka Serikali Kuu ikiwa ni mchango wa ujenzi wa bweni la wavulana wenye mahitaji maalum.



Wanafunzi wa shule ya msingi Ikwete wakiwa katika darasa jipya shule ya msingi Ikwete

Hivyo,katika kipindi cha miaka 3 ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Halmashauri ya Mji Makambako katika divisheni ya elimu ya awali na msingi jumla ya madarasa 113 yamejengwa na kupunguza upungufu wa madarasa kwani jumla ya madarasa yanayohitajika ni 694 yaliyokuwepo ni 357 na pungufu yalikuwa madarasa 337 na kwa sasa pungufu ni madarasa 224.



# MIAKA 3 YA
# DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
# HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO





MADARASA 2 NA OFISI 1 SHULE YA MSINGI MAKAMBAKO(SHULE KONGWE)

Aidha,Kupitia miradi hiyo jumla ya Matundu 129 ya vyoo yamejengwa na kupunguza upungufu wa matundu ya vyoo kutoka matundu ya vyoo 459 hadi kuwa na upungufu wa matundu 330 kwa ajili ya wanafunzi wavulana na wasichana,matundu ya vyoo kwa ajili ya wavulana yanayohitajika ni 590 yaliyopo ni 483 na pungufu kwa sasa ni matundu 107 na wasichana mahitaji ni matundu 764 yaliyopo ni 541 pungufu ni 223.



# MIAKA 3 YA
# DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
# HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



## KITENGO CHA TASAF



BWALO LA CHAKULA NA JIKO - SHULE YA SEKONDARI MLOWA

**Na. Lina Sanga**

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri ya Mji Makambako kupitia Kitengo cha TASAF imepokea jumla ya Bil. 1.67 ya utekelezaji wa miradi 19 ya miundombinu ya Afya na elimu ambapo miradi 17 imekamilika,miradi 2 ipo hatua ya ukamilishaji.







Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa bweni la wavulana katika shule ya sekondari Mtimbwe ambapo jumla mil. 91.4 zimetumika na ujenzi umekamilika,ujenzi wa bweni la wavulana shule ya sekondari Kitandililo mil. 135.6 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi ambapo kwa sasa ujenzi upo hatua ya ukamilishaji na Mil. 98.3 zimetumika katika ujenzi wa bwalo la chakula na jiko katika shule ya sekondari Mlowa na ujenzi wa mradi huo umekamilika.



BWENI LA WAVULANA SHULE YA SEKONDARI MTIMBWE

Katika divisheni ya elimu ya awali na msingi kupitia TASAF katika shule ya msingi Ubena jumla ya mil 92.4 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 3 na matundu 6 ya vyoo ujenzi umekamilika,katika shule ya msingi Magomati







kijiji cha Usetule mil.184.8 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 6,ofisi na matundu 12 ya vyoo ,ujenzi wa madarasa 5,ofisi na matundu 12 katika shule ya msingi Makatani jumla ya mil. 133.9 zimetumika,na mil 133.9 zilitolewa shule ya msingi Magongo kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 5,ofisi na matundu 12 ya vyoo na majengo hayo yanatumika.

Aidha,katika kituo cha Afya cha Ikelu jumla ya Mil. 66.9 zimetumika katika ujenzi wa nyumba pacha za watumishi,mil.91.9 zimetumika katika ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na wodi la mama na mtoto mil. 84.5 ujenzi umekamilika na mradi unatumika na mil. 120.5 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto awamu ya pili, ujenzi upo katika hatua za ukamilishaji.



KITUO CHA AFYA CHA IKELU,JENGO LA OPD NA WODI YA MAMA NA MTOTO







Lakini pia, katika Zahanati za Vijiji vya Ngamanga,Ibatu,Nyamande na Ikwete TASAF imetekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba pacha za watumishi ambapo kila zahanati ilipokea mil. 92.4 na nyumba za watumishi katika zahanati ya Nyamande,Ikwete na Ibatu ujenzi umekamilika na katika zahanati ya Ngamanga ujenzi upo hatua ya ukamilishaji.




NYUMBA PACHA YA WATUMISHI (2IN 1) KITUO CHA AFYA IKELU



# MIAKA 3 YA
# DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
# HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



## SEKTA YA BARABARA – WAKALA WA BARABARA MIJINI NA VIJIJINI (TARURA)



BARABARA YA KIWANGO CHA LAMI MTAA WA AZIMIO

**Na. Lina Sanga**

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kuu kupitia mfuko wa barabara iliidhinisha jumla ya bil. 2.8 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za matengenezo ya barabara na madaraja,katika maeneo ya Mjini na Vijijini ndani ya Halmashauri ya Mji Makambako.

Kati ya fedha hizo jumla ya mil. 831 ni fedha kwa ajili ya matengenezo ya

**MIAKA 3 YA**
**DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**
**HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO**





barabara,bil. 1 ni fedha za maendeleo ya mfuko wa jimbo na bil. 1 ni fedha za tozo ya mafuta kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilomita 3,kiwango cha changarawe kilomita 10,matengenezo ya kawaida kilomita 34.88,matengenezo ya kuimarisha sehemu korofi kilomita 56.02,matengenezo ya muda maalum kilomita 4.05,matengenezo ya madaraja mawili na ujenzi wa makalavati.



UJENZI WA DARAJA LA GOLIGOTHA KATIKA BARABARA YA A-ONE -DS



# MIAKA 3 YA
# DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
# HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



## PICHA ZA MIRADI



BWENI MOJA PACHA (2 IN 1) KATI YA MAWILI YA WATOTO WENYE MAHITAJI MAALUM SHULE YA MSINGI IDOFI



BARABARA YA MADUNDA(MJIMWEMA) YENYE KIWANGO CHA LAMI NA MATAA



# MIAKA 3 YA
# DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
# HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO





SHULE YA SEKONDARI YA KITISI



SHULE MPYA YA SEKONDARI YA MBUGANI -KITANDILILO



# MIAKA 3 YA
# DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
# HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO





SHULE YA MSINGI MPYA YA AZIMIO ILIYOJENGWA KUPITIA MRADI WA BOOST



# MIAKA 3 YA
# DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
# HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO






GARI MPYA YA WAGONJWA ILIYOTOLEWA NA SERIKALI ILI KUPUNGUZA UHABA WA GARI LA WAGONJWA,KWA SASA HALMASHAURI INA MAGARI MAWILI





# MIAKA 3 YA
# DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
# HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO





SOKO KUU LA MAZAO LA HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO LILILOPO MTAA WA MAKATANI(KIUMBA) KATA YA LYAMKENA





# MIAKA 3 YA
# DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
# HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



MASAA YA KAZI NA POSTIKODI YA OFISI ZA HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO








# MIAKA 3 YA
# DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
# HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



**JARIDA HILI NI JARIDA MTANDAO,LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO YA SERIKALI KATIKA HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO,TUFUATILIE KWENYE TOVUTI YETU NA MITANDAO YA KIJAMII IFUATAYO;-**

**www.makambakotc.go.tz**

**makambakotc**

**Makambako Town Council**

**makambakotc**

**makambakotc**

**follow us and subscribe in our youtube channel**

JARIDA LA MIAKA 3 YA DKT. SAMIA.indd 18 3/25/2024 1:45:38 PM